

# Tusome Kikabwa



Ni rahisi kusoma Kikabwa



SIL International

Huduma ya Kutafsiri Biblia katika Lugha za Asili Mkoa wa Mara  
SLP 1235  
Musoma, Tanzania



# Tusome Kikabwa



Ni rahisi kusoma Kikabwa



SIL International

Huduma ya Kutafsiri Biblia katika Lugha za Asili Mkoa wa Mara  
SLP 1235  
Musoma, Tanzania

**Kichwa:** Tusome Kikabwa  
**Lugha:** Kikabwa na Kiswahili  
**Waandishi:** Paul Meja, John Masige  
**Mshauri:** Leila Schroeder  
**Kimetolewa na:** Huduma ya Kutafsiri Biblia Katika Lugha za Asili, Idara ya Literacy  
**Michoro:** International Illustrations, The Art of Reading, 2.0,  
© SIL International, 2001

Mfumo huu wa maandiko ni majaribio. Kama una maoni au mapendekezo, wasiliana nasi kwa anwani ifuatayo:  
Huduma ya Katafsiri Biblia katika Lugha za Asili  
S.L.P. 1235, Musoma, Tanzania

© SIL International, 2011, Toleo la Pili



## **Utangulizi**

Uhaliya, uasilia na utamaduni wa lugha yetu umekuwa ukipotea siku kwa siku kwa sababu ya kutokuwa na vitabu au kitabu kilichoandikwa katika lugha yetu. Na hata kama vimekuwapo, basi hakuna mtu aliye na uwezo wa kuvisoma.

Kwa hali hiyo basi, ***Huduma ya Kutafasiri Biblia katika Lugha za Asili Mara***, inajitoa na kufanya kazi ya kufundisha watu kusoma na kuandika katika lugha zao.

“**Tusome Kikabwa**” ni kitabu cha mwanafunzi kinacholenga kumsaidia mzawa na mtumiaji wa lugha ya Kikabwa kusoma na kuelewa katika lugha yake.

Kitabu hiki kimeandaliwa na ***Huduma ya Kutafasiri Biblia katika Lugha za Asili Mara***; ni kitabu kitakachowasaidia watu wa lugha yetu, wanaojua kusoma na kuandika katika lugha ya Kiswahili, kusoma na kuielewa lugha yetu bila shida.

Kitabu hiki kimekusudiwa kutumika katika semina mbalimbali za kisomo na hata kwa mtu binafsi kujisomea mwenyewe nyumbani na hata akiwa safarini.

Masomo katika kitabu hiki yamepangwa katika mpangilio mzuri utakaomsaidia mwanafunzi kujifunza kusoma hatua kwa hatua lugha yake bila shida yoyote. Na kila somo linayo mazoezi ambayo yatamsaidia msomaji kujipima uwezo wake wa kusoma na kuielewa lugha yake kwa usahihi. Majibu ya kila zoezi yanapatikana mwishoni mwa kitabu hiki.

Ni rahisi kusoma Kikabwa!

Waandaaji wa kitabu hiki wanakutakia Baraka za Mungu unaposoma na kutumia Kikabwa!



## 1. Herufi za lugha yetu zifananazo na zile za Kiswahili


Herufi hizi hazitakuwa ngumu kwako kujifunza. Ni zile zile katika lugha zote. Hebu sasa na tufanye mazoezi ya kusoma herufi zifuatazo.

Irabu: **a, e, i, o, u**


Konsonanti: **ch, d, g, h, j, k, m, mb, n, ng', ny, r, s, sh, t, w, y**




orurimi




nyamuhu




ekigu




omururo




erimiro




ekinyonyi



ekisasi



eguruki



eng'iti


## 2. Herufi ambazo hazimo katika Kiswahili

Herufi hii itakuwa ni mpya kwako. Luga yetu inahitaji herufi za ziada ili iweze kuandikwa kwa usahihi. Herufi hiyo mpya ni hii ifuatayo.


Irabu mpya: **bh**




okusabha




endobho




bhutuku



okwisabha



embebha



obhuriri


Andika neno la Kikabwa kulia chini:

Kiswahili	Kikabwa
uji	
uso	
nje	
ardhi	
mchana	


### 3. Irabu ndefu

Katika lugha yetu tuna aina mbili za irabu, irabu fupi na irabu ndefu. Katika Kiswahili kuna aina moja tu. Tunaandika irabu ndefu kwa kuandika irabu pacha zinazofanana kwa pamoja. Unachotakiwa kufanya ni kusoma / kutaja irabu hiyo kwa muda mrefu kidogo. Kufanya hivyo inatusaidi kutofautisha maneno ‘erigoti’ (shingo) na ‘erigooti’ (kodi).


Irabu ndefu: **aa, ee, ii, oo, uu**




ebhikaai




omukeeka



eriiso




ekimoori



emiguuwa

Oanisha maneno yafuatayo na picha yake hapo chini:

obhubhere obhubheere okutuura okutura oruji oruuji




#### 4. Herufi mwambatano: W


Kiswahili kina konsonanti zinazofanya kazi pamoja na kufanya sauti. Lugha yetu inafanya hivyo pia. Tuone ni herufi zipi zinazofanyakazi pamoja katika lugha yetu.

Herufi zenyewe W mbele yake:


**bhw, gw, hw, jw, kw, mw, nw, ngw, nyw, rw, sw, tw**




omugi **gwani**




omweri



okutwi



omubhwimi



omukwami

Jaza nafasi zilizo wazi kwa kuandika herufi zinazokosekana.


oku\_\_\_\_i



o\_\_\_\_eri



egin\_\_\_\_i



## 5. Herufi mwambatano: Y


Tuone herufi nyingine zinazofanyakazi pamoja.

Herufi zenyewe Y mbele yake:


**dy, gy, hy, jy, ky, my, ng'y, ry, sy, ty**




**ekisyusu**



**entyenyi**




**ekyeyo**



**eryubha**



**okwobhohya**



**okuriisya**

**Jaza nafasi zilizo wazi kwa kuandika maneno katika lugha yako yenye maana ya hayo ya Kiswahili.**

paji la uso

eki\_\_\_\_\_usu

kutwisha

okwiti\_\_\_\_\_a

kusaga


oku\_\_\_\_\_a

## 6. Herufi mwambatano: N


Tuone herufi nyingine zinazofanyakazi pamoja.

Herufi zinazotanguliwa na N:


**nch, nd, ng, nk, ns, nt**




erigongoro



entikiri




omugongo



enchupa



omugunda



egindaara

Jaza nafasi zilizo wazi kwa kuandika maneno katika lugha yako yenyewe maana ya hayo ya Kiswahili.

mlima

e \_\_\_\_ uku

simba

e \_\_\_\_ wi

nywele

egi \_\_\_\_ ukya

## 7. Herufi nyingine ambazo hazimo katika Kiswahili

Herufi hizi zitakuwa ni mpya kwako. Lugha yetu inahitaji herufi za ziada ili iweze kuandikwa kwa usahihi. Tazama apostrofi (') inatofautisha sauti n'y na ny.


Herufi mpya: n'y



okunen'ya



okuhon'ya



okuhwen'ya

**Tazama apostrophe (')**  
inaotofautisha sauti hizi na  
hizo za kulia:

okunen'ya (kunyonyesha)  
okuhon'ya (kutembeza)  
okuhwen'ya (kuponya)

**Tazama sauti ya ny ni**  
kawaida kwako na ni tofauti  
na sauti hizo kushoto:

okukenya (kukimbia)  
okumenya (kuishi)  
okukunya (kufyeka, kukunja)


Chagua neno sahihi kati ya haya yafuatayo.

ny au n'y

kugusa      okukunya    au    okukun'ya

kutaga      okunya      au    okun'ya

kukimbia    okokenya    au    okuken'ya



## 8. Maneno yanayowakilisha mahali —Nomino

Katika lugha ya Kikabwa kuna maneno mafupi yanayowakilisha mahali, yaani ni **ku na mu**, ambayo hutangulia nomino.

Tazama kistari (-) kinachotenga maneno yanayowakilisha mahali. Kwa mfano:

Abhantu bharingi **mu-matoka**;  
ematoka eringi **ku-njira**.



**Unganisha kirai cha Kiswahili na tafsiri yake kwa kuchora mistari:**

ndani ya sufuria	mu-nkuku
juu ya nyati	mu-kifurira
mjini	mu-shure
shuleni	mu-mugi
mlimani	ku-ngaji ya kabhiri
kwenye ngazi ya pili	ku-ng'era

**Jaza nafasi zilizoachwa wazi hapo chini kwa kutumia maneno ya Kikabwa.**

katika mzinga **mu-mutana**


kwenye kisu **-kigeso**

mjini **-mugi**

#### **9. Maneno yanayowakilisha mahali —Vitenzi**

Pia kuna maneno madogo mengine yanayowakilisha mahali ambayo hufuatia vitenzi, yaani **ko, mo, yo, ho**.

Tazama kistari (-) kinachotenga maneno yanayowakilisha mahali. Kwa mfano:



Erituko rinu ndahamba-**mo** embusiro.

**Unganisha kirai cha Kiswahili na tafsiri yake kwa kuchora mistari:**

hajampata hapo	areeri-mo
wanachuma humo	atamunyooreri-ho
imeanguka humo	bhanikiri-ko
wanapita juu	egwiri-mo
amelala humo	bharaha-mo
wameanika juu	bharahita-ko

**Jaza nafasi zilizoachwa wazi hapo chini kwa kutumia maneno ya Kikabwa.**

panda juu	tira-_____
toa hapo	rusya-_____
wanaenda kule	bharagya-

## 10. Kitenzi shirikishi

Kitenzi shirikishi “ni” katika lugha yetu ni kaneno kadogo; sio rahisi kwa neno hili kujitegemea. Tazama kistari hicho (-) kinachofuata kitenzi shirikishi katika Kikabwa:

Wunu m-murimi. Huyu ni mkulima.

Gunu m-mutana. Huu ni mzinga.


Rinu ni-riguha. Huu ni mfupa.

Ganu m-maguha. Hii ni mifupa.

Yinu ni-nkoko. Huyu ni kuku.

Ginu ni-ginkoko. Hawa ni kuku.

Runu n-dusara. Hili ni paa.



**Jaza nafasi zilizoachwa wazi hapo chini kwa kutumia  
lugha yetu ya Kikabwa.**


Uuwe m-musaani waani.

Irya \_\_\_\_-ntari yaani ehya.

Kinu \_\_\_\_-kigeso kyaho.

## 11. Hadithi ya Kikabwa

### Erigano rya kinú Manga Yaarora mu-Riihe



Akare hayo, yaaringa-ho omuntu umwi. Omunto uyo, yaabhirikirwanga Manga. Orusiku rumwi, yaagya mu-riihe hamwi na abhasirikare abharikyaye mu-nkuku indi. Enkuu iyo yaabhirikirwanga ega, Ku-rirangi. Hanu bhaahika mu-nkuku muyo, bhakaamba okurwana erihe. Bhakarwana, bhakarwana, bhakarwana. Bhakahigwa kwa okubha bheeki bhaaringa na amata, emisimu, egimunga na amapanga, nawe abhasigu bhabho bheeki bhaaringa na embunde na amatimu.

Mbe bhoono, bhaaja okuhigwa, bhakatuna ekisaka bhakeekara-mo, naho bhaamure kinú bharaakore. Bhatareeseemya ego, embunde ekagamba ega, "Gunguruuu!" Hanu yaagamba, bhonsegó bhakarara hansi. Kumbe, abhasigu bhabho bhabharuji kya ego bhareeri. Kimwi abhasigu bhayo bhonse bhakagunya mu-bhisaka.

Mbe mura, niigo abhasirikare bha omukaruka uyo Manga bheemuka ego, tigana bhaasunyuntirwa amarisaasi kya embura. Bhonsegó bhakahwera hansi. Omukaruka uyo Manga omwene ego, ng'o yaatigara yeemiriri, wonse akarora kinu ni ki, ndeegwa amang'ana gakong'eri. Kimwi akagamba ega, "Tiga nigwisye hansi, niibhurubhunge mu-manyinga, nikorye muna ndasirwe nkwiri." Kimwi akagwa hansi, akeebhurubhunga

mu-manyinga omubhiri omugima na mu-bhusu bhonsego,  
kimwi akaterema.

Mbe, abhasigu bhakaaja bhakahika harya. Hanu yaabheegwa, yaakeerya Waryubha ega, “Mbikira omoyo gwani okwamba, bhanu bhagye.” Kimwi gukahwa-mo. Mbe, abhasigu bharya bhaamutajataja. Hanu bhaamara, bhakagamba ega, bhanu tubhamariri, bhakagya.

Manga hanu yaatuumma-yo, yaamagamaga enu na enu, hanu yeegwa kirikiri, yaakurumuka okurwa hayo, kya eriiguge rirasirwe ku-roototi. Yaatiimura oruteeri okuhinda iika, kya enungu eragya okutuurya abhaana bhaaye. Hanu yaahika iika, akeehiimiriry ega, atakyagya mu-riihe kweki. Mbe, kiyo nkyo Manga yaarora mu-riihe.

Erigano ryani rihwereri hayo.

## **12. Methali za Kikabwa**

**Abhakuru bhaagamba ega...**

- 1. Nyambisa obhurweri, ekiriro kirimubhuura.**
- 2. Kiringi embere kitakubhuna bhigoti.**
- 3. Nyamugya ng'ora, yeeta kinú kirakenya.**
- 4. Hanu yaniiri, nho erakamirwa.**
- 5. Eng'ombe enkangati ng'yo eranywa amanji amarabhu.**
- 6. Nyakimamaano yaarya amakeega.**
- 7. Nyamuhaana kake, atang'ana nyamurungusirya.**
- 8. Nyantagererwa yaatuura ekihuuri egembe.**
- 9. Bhuriibhwa eng'ombe, bhutang'ana bhuriibhwa eng'era.**




## 13. Majibu ya Masomo

Linganisha na rekebisha majibu yako na majibu sahihi yafuatayo.

### Somo la 2      Somo la 3

obhusara  
obhusu  
kibhara  
erirobha  
omubhasu



### Somo la 4

okutwi  
omweri  
eginkwi

### Somo la 5

ekisyusu  
okwitikya  
okusya

### Somo la 6

enkuku  
endwi  
egintukya

### Somo la 7


okukun'ya  
okun'ya  
okukenya

### Somo la 8

ndani ya sufuria	mu-nkuku
juu ya nyati	mu-kifurira
mjini	mu-shure
shuleni	mu-mugi
mlimani	ku-ngaji ya kabhiri
kwenye ngazi ya pilii	ku-ng'era

**mu-mutana**  
**ku-kigeso**  
**mu-mugi**

### Somo la 9



tira-**ko**  
rusya-**ho**  
bharagya-**yo**

### Somo la 10

Uuwe **m**-musaani waani.  
Irya **ni**-ntari yaani ehya.  
Kinu **n**-kigeso kyaho.

**Umefanyaje? Hongera kwa kusoma lugha yetu!**





## **Kuhusu Huduma**

Huduma ya Kutafsiri Biblia katika Lugha za Asili ilianza mwaka 2005 katika mkoa wa Mara. Huduma hii ilianza kwa ushirikiano uliofanywa kati ya viongozi wa makanisa na mashirika mbalimbali na **SIL International**. Huduma hii inashirikiana na huduma za Kikristo kama vile Chama Cha Biblia cha Tanzania na Life Ministry, pamoja na madhehebu zaidi ya 30 ya Kiprotestanti, Kipentekoste, Kiadventisti, na Kikatoliki.

Huduma hii inafikisha Neno la Mungu kwa makabila mbalimbali katika lugha zao za asili kwa imani ya kwamba Mungu anaongea lugha zote!

**Serikali ya Tanzania inathamini lugha za asili. Sera ya Utamaduni inasema hivi:**

*Lugha za jamii ni hazina kuu ya historia, mila, desturi, teknolojia na utamaduni wetu kwa jumla. Aidha, lugha hizi ni msingi wa lugha yetu ya taifa, yaani Kiswahili. (3.2. Lugha za Jamii)*

Huduma ya Kutafsiri Biblia inasaidia katika: kufanya utafiti wa isimu, kutafsiri maandiko mbalimbali pamoja na Biblia, kuanzisha na kuendeleza alfabeti na mifumo ya uandishi, kuanzisha mpango wa kusoma na kuandika, na kuhimiza matumizi ya Biblia.



Huduma ya Kutafsiri  
**BIBLIA KATIKA LUGHA ZA ASILI**  
Mara, Tanzania